
OFISI YA MWANASHERIA
MKUU WA SERIKALI

# WIKI HII MAGAZETINI NA MITANDAONI

31/03/2025 ► 04/04/2025

OAG



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari (katikati) akishuhudia Naibu Mwanasheria Mkuu, Samwel Maneno (kushoto) na Mtendaji Mkuu wa Baraza la Taifa la Ujenzi, Matiko Mturi wakibadilishana mkataba baada ya kuingia makubaliano ya ushirikiano wa kitaalamu katika sekta ya ujenzi, Dar es Salaam jana. (Picha na Rahel Pallangyo).

# Mwanasheria Mkuu, baraza kushirikiana sekta ya ujenzi

Na Zena Chande

OFISI ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Baraza la Taifa la Ujenzi wamesaini makubaliano ya kushirikiana kitaalamu katika sekta ya ujenzi.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari amesema wamesaini makubaliano hayo kwa sababu taasisi hizo zinashabihiana kwenye suala la ujenzi na hasa katika miradi ya kimkakati.

Johari aliwaeleza waandishi wa habari Dar es Salaam jana kwa kuzingatia makubaliano hayo wanatarajia kuboresha ujuzi na umahiri katika mikataba ya ujenzi.

"Tumeshuhudia serikali ya Awamu ya Sita ikiendelea na jitihada zake za kufanya miradi mbalimbali mikubwa mikubwa na ya kimkakati ya ujenzi, kwa hiyo sisi kama wanasheria, wataalamu wa ujenzi tunatakiwa kuhakikisha tunakuwa na ujuzi na utaalamu stahiki kuhakikisha miradi hii ya ujenzi mikubwa mikubwa inafanyika vizuri na mikataba inaandaliwa vizuri, inatekelezwa vizuri na usimamizi wake unakuwa mzuri," alisema.

Alisema wataalamu wa ujenzi katika Baraza la Taifa la Ujenzi na wanasheria kwa upande wa ofisi yake, lazima wafanye kazi kama timu kama kweli wanataka kuhakikisha mikataba ya ujenzi na taaluma yake inafanyika vizuri.

"Ni jambo ambalo tunaamini tukilifanya tukiwa na hati hii ya makubaliano tutaweza kubadilishana wataalamu na kwa kufanya hivyo wataalamu wetu watafahamu masuala haya yanayohusiana na sekta ya ujenzi kwa kina zaidi," alisema.

Alisema anataka wabadilishane utaalamu kwa kupata ushauri wa kitaalamu katika masuala yote yanayohusu sekta ya ujenzi.

"Lakini pili nilizungumza kwenye mafunzo yetu kule Arusha kwamba mafunzo tunakwenda kuyapa kipaumbele kikubwa sana, na mafunzo yapo ya aina mbalimbali mojawapo ni kubadilishana kama hivi kwa kushirikiana na taasisi nyingine ambao wao wana ubobezi kwenye eneo Fulani," alisema.

Aliongeza: "Tunabadilishana wataalamu na kwa kufanya hivyo unajikuta wataalamu wako wanapata mafunzo stahiki kwa maana wa pande zote mbili Baraza la Taifa la Ujenzi wanapata mafunzo ya kile tunachofanya na sisi tunapata uzoefu wa kile wanachofanya."

Alisema jambo lingine ni kushirikiana kufanya uchambuzi wa madai yatokanayo na mikataba ya ujenzi na suala la majadiliano ya mikataba ya ujenzi.

"Kwa sababu mikataba ya ujenzi iko tofauti kidogo na mikataba ya huduma, tukae pamoja tuone ni vitu gani tunapaswa kuvizingatia katika mikataba ya ujenzi ili kuhakikisha mkataba huo unakaa vizuri sababu wakati wa utekelezaji wake unaweza kujikuta unakwama kumbe kwenye majadiliano haukuzingatia vitu muhimu matokeo yake ukazaa mkataba ambao hauna vile vitu vya msingi ambavyo Baraza la Taifa la Ujenzi linavifahamu na linasisitiza vizingatiwe katika mikataba ya ujenzi," alisema.

Aliongeza: "Lakini na usuluhishi wa migogoro pia ya mikataba ya ujenzi na yenyewe ina upekee wake ambao sisi tunaamini ni muhimu sana tukayafahamu na masuala mengine mtambuka yanayozingatia sekta ya ujenzi nchini na mambo mengine katika sekta ya sheria ili tushirikiane vizuri".

Akilizungumzia hilo Mtendaji Mkuu wa Baraza la Taifa la Ujenzi, Matiko Mturi alisema makubaliano hayo ni fursa kubwa kwao kujifunza na kuchota ujuzi wa kisheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

"Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiyo inayosimamia na kuhakikisha mikataba yote ya Tanzania iko vizuri na mojawapo ni mikataba ya sekta ya ujenzi kama mnavyojua sasa hivi kuna mikataba mingi ya miradi mikubwa kwa hiyo lilipokuja wazo la kushirikiana tuliona linaoana kabisa na azma yetu ya kuhakikisha miradi ya sekta ya ujenzi inatekelezwa vizuri," alisema.

Home About Us Privacy Policy Contact Us

DIRAMAKINI ARTICLES LOCAL NEWS INTER NEWS ADVERTS NEWSPAPERS PHOTO EVENTS

Home > Habari

FOLLOW US

# Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,Baraza la Taifa la Ujenzi zaingia makubaliano

**DAR-Ofisi** ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Baraza la Taifa la Ujenzi zimeingia makubaliano kwa ajili ya ushirikiano wa kitaalamu katika Sekta ya Ujenzi.



Akizungumza na waandishi wa habari Jijini, Dar es Salaam tarehe 03 Aprili, 2025 Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari amesema kuwa wameingia makubaliano hayo kwa sababu taasisi hizo zinashabihiana kwenye suala la ujenzi na hasa katika miradi mikubwa ya kimkakati.

itvtz




202 5

itvtz #HABARI: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Baraza la Taifa la Ujenzi zimeingia makubaliano kwa ajili ya ushirikiano wa kitaalamu katika Sekta ya Ujenzi.

**Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Ser...**
@Oag_tz

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Baraza la Taifa la Ujenzi zimeingia makubaliano kwa ajili ya ushirikiano wa kitaalamu katika Sekta ya Ujenzi.



Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Ser...
@Oag_tz



# TUPO KARIBU YAKO!

**Tufuatilie kupitia**

oagtanzania

info@oag.go.tz

www.oag.go.tz

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Mtumishi
Mji wa Serikali Mtumba
S. L. P 630
Dodoma - Tanzania

**KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188**

Weledi na Ubora